

Mji wa Pittsburgh umetangaza vikwazo zaidi katika kujitenga kijamii

PITTSBURGH, PA (Machi 30, 2020) Mji wa Pittsburgh umetangaza kufunga viwanja vyake vya mpiwa wa vikapu na unatazamia kutekeleza kanuni za kujitenga kijamii ambazo ni muhimu kupambana na janag la virusi vya COVID-19 .

Wakati wakazi wa Pittsburgh wamekuwa wakizingatia kwa kiasi kikubwa maelekezo ya kukaa angalau miguu sita kutoka kwa wengine ili kupunguza kuenea kwa virusi, wengine hawajatilia maanani jambo hilo, hasa katika mbuga za mji.

Mbuga zitanabakia wazi, na wakazi wanahimizwa kuzitumia kukuza shughuli za kimwili. Lakini kuanzia leo, wafanyakazi wa kazi za umma wanaondoa vifaa vya mpira wa vikapu kutoka kwenye uwanja na kufunga sehemu ya mtazamo kwenye mlima Washington. Maeneo hayo yalikuwa yamejaa mwishoni mwa wiki na wakaazi ambao hawakuwa wanafuata sheria za kujitenga kijamii.

Michezo ya vikundi hairuhusiwi katika mbuga za jiji. Mbali na kufunga uwanja wa mpira wa kikapu, maafisa wa usalama wa umma watakuwa wanafuatilia viwanja vya soka na maeneo mengine ya kucheza ili kuhakikisha sheria za kujitenga za kijamii zinafuatwa. Uwanja mmoja wa soka katika Mbuga ya Mwoneko wa mito tayari umefungwa.

Uga za michezo tayari zimefungwa, lakini baadhi yao zinaendelea kuruhusu watoto kuzitumia: wakazi wanakumbushwa kwamba vifaa vya Hifadhi na hali za kucheza zinaweza kosa kuwa salama, kwa sababu virusi vya COVID_19 vinaweza kuishi kwa sakafu kwa siku kadhaa.

Wakazi wanapaswa pia kudumisha kujitengaya kijamii wakati wa kutumia njia za hifadhi, ambazo zimekuwa na watu wengi sana katika siku za hivi karibuni.

Maafisa wa usalama wa umma wanaongeza juhudi za kuhimiza tabia ya kuwajibika. Polisi wa bustani na polisi wa kawaida wanalinda doria kwenye mbuga kwa karibu zaidi na kutoa vikumbusho ya kujitenge sahihi kijamii, na wafanyikazi wa umma waweka ishara zaidi ya kuwakumbusha watumiaji wa hifadhi na uwanja wa michezo kuhusu kufungwa huko.

Wakazi wanakumbushwa zaidi kutokushiriki chakula na wafanyikazi wa usalama wa umma na wafanyakazi wengine wa mji. Wakati matoleo hayo ni wazi kuwa ya nia bora ya kuonyesha msaada kwa wafanyakazi katika nyakati hizi ngumu, hatari ya kueneza ugonjwa miongoni mwa wafanyakazi wa jiji ni kubwa sana, na wakazi wanaombwa kuchangia chakula kwa sehemu nyingine maalumu.

Kukaa nyumbani, kufanya mazoezi ya kujitenga kijamii wakati wa kutembea nje na kuosha mikono ni sehemu muhimu ya mapambano dhidi ya janga la kimataifa la COVID-19. Kwa kufanya sehemu yao wakaazi wa Pittsburgh wanaweza kusaidia kusitisha kuenea kwa ugonjwa huo na kupunguza mizigo kwa wafanyakazi wa hospitali na maafisa wa usalama wa umma katika mistari ya mbele ya mapigano kwa ajili yetu sote.

Mawasiliano:

Timothy McNulty, Mkurugenzi wa mawasiliano, Timothy.McNulty@pittsburghpa.gov

Chris Togneri, Ofisa habari wa umma, PIO@pittsburghpa.gov